# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**ALLIANCE GIRLS HIGH SCHOOL**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 2**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

**ALLIANCE GIRLS HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016**
**102/2**
**Karatasi ya 2**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**UFAHAMU**

a). Maendeleo / Jinsi ya kuleta maendeleo (alama 1)

b). Hulka ya kutarajia mambo mazuri zaidi maishani. (alama 2)
wanafanya kazi kufa kupona na kuwa na matumaini ya kuishi vizuri zaidi kesho

c). Jinsi serikali iliyo na uwezo wa kutekeleza ndoto zake

i). Inafanya mipango ya kuleta hali bora kwa

ii). Kushirikisha wadau ambao wana majukumu ya kusimamia na kutekeleza mipango katika muda unaotakiwa.

iii). Inatumia rasilimali zake k.v. madini, misitu, ardhi (alama 3×1 = 3)

d). i). Uvivu / Kutopenda kujishughulisha na kazi
ii). Kuelekezeana lawama / Kuegemea zaidi katika kujadili udhaifu badala ya kujadili namna ya kuboresha hali. (alama 2× 1= 2)

e). Wito wa aya ya mwisho
Tuyachunguze mambo yaliyotuangusha na kuketi chini kuyajadili wazi, tukemeane na kurekebishana bila hofu. (2×1= 2)

F). Methali zinazohusiana na aya mbili za mwisho
i) Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu
ii). Jifya moja haliinjiki chungu (2 × 1 = 2)

g). i). kukidhi haja - kutosheleza mahitaji / timiza matakwa
ii). kiu ya maendeleo – uchu wa kuwa na maendeleo / haja
iii). Tunyosheane vidole usoni – tukemeane / tuonyane (3 ×1 = 3)

**MUHTASARI**

A). Changamoto zinazoikumba lugha ya kiswahili kama lugha rasmi.
-Lugha ya kiswahili kushindania nafasi sawa na ile ya kiingereza katika shughuli za kikazi.
-Lugha ya Kiswahili itachukua nafasi ipi na kiingereza nacho kichukue ipi.
-Kiwango cha maandalizi ya wananchi katika kuyapokea mabadiliko haya
-Kufanyika kwa uandishi wa vitabu zaidi vya Kiswahili
-Mtazamo hasi wa wananchi kuwa kiswahili ni lugha ngumu
-Utoaji wa nafasi finyu kwa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wazungummzaji ambao huzionea lugha za kigeni fahari
-Kuharibiwa kwa Kiswahili na sheng au lugha za kienyeji
Hoja 6 × 1 = alama 1 mtiririko =7

b). Namna ya kuimarisha matumizi ya Kiswahili nchini
- Watunga sera kueleza kinagaubaga mawanda ya matumizi ya lugha hizi mbili kazini.
- Watumishi wa umma wapewe mafunzo maalumu kuhusu mbinu za mawasiliano katika Kiswahili
- Vyuo vikuu na taasisi za mafunzo kuwaandaa wanafunzi wao wapya kuhusu mahitaji mapya ya kikatiba
- Wanaohusika na utekelezaji wa sera wapate mafunzo kutoka kwa wataalamu wa Kiswahili
- Kuandikiwa kwa vitabu zaidi vitakavyofunza mbinu za mawasiliano.
- Wananchi wahimizwe kukionea fahari Kiswahili, wakipende na kukielewa
- Viongozi wawe vielelezo kwa kukizungumza Kiswahili sanifu .
- Viongozi wapewe kipaumbele katika kufunzwa kwa Kiswahili

Hoja 7 × 1 = 7 Utiririko1 Jumla alama 8

**MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

(a) Andika vigezo vitatu vinavyotumiwa katika kuainisha irabu (alama 3

- Sehemu ya ulimi
- Mwinuko wa ulimi
- Mkao wa midomo

(b) (i) Eleza maana ya mofimu. (alama 2)

Kipashio kidogo kabisa cha lugha chenye maana ya kisarufi.

(ii) Toa mfano mmoja mmoja wa mofimu huru na mofimo tegemezi. (alama 2)

Huru – Baba dirisha n.k

Tegemezi – Mtoto, a-na-chek-a, madirisha

(c) Kwa kutoa mifano onyesha majukumu manne ya viambishi awali. (alama 2)

(i) Nafsi mf. Nitasoma

(ii) Wakati/hali mf – ta,me

(iii) Ngeli mf kitaoshwa

(iv)- umoja na wingi – mtu – watu

(v) - kirejeshi - atakayesoma

(vi) Ukanusho – hakusoma

(vii) Mtendwa - atatupiga

(d) Tunga sentensi ukitumia nomino katika ngeli ya I-ZI kudhihirisha ukubaliano wa kisarufi. (alama 2)

Sahani ilioshwa na mama

Sahani zilioshwa na mama

(e) Yakinisha sentensi ifuatayo katika wingi. (alama 2)

Mtu asiyeugua anahitaji daktari.

Watu wanaougua wanahitaji madaktari.

(f) Andika vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendeana (alama 2)

- La - liana
- nywa - nyweana

(g) Bainisha yambwa tendwa na yambwa tendewa katika sentensi hii. (alama 2)

Ninamtaka mwanafunzi aniandikie barua.

yambwa tendwa – barua

tendewa - mimi

(h) Tambua aina ya vishazi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Tulimtembelea alipokuwa mgonjwa.

(i) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale. (alama 4)

Wale wazuri sana watatuzwa zawadi nyingi.

S → KN + KT
KN →W + V + E
W → Wale
V →Wazuri
E → Sana
KT →T + N + V
T → Watatuzwa
N → zawadi
V → nyingi

(j) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo (alama 2)

Mtoto anapendezwa na ziwa

Mtoto anapendezwa na titi.

Mtoto anapendezwa na sehemu yenye maji.

(k) Andika sentensi tatu zenye kudhihirisha matumizi mbalimbali ya KI. (alama 3)

Sentensi zionyeshe maana zifuatazo

(i) udogo mf kitoto
(ii) wakati – alikuwa akisoma
(iii) ngeli (ki – u) kitabu kime
(iv) Ki mfanano – kizee, kinyama zozote
(v) Utanusho – hakiliki
(vi) Kiwakilishi cha ngeli ya ki-vi mfano kilianguka.

(l) Andika kwa usemi wa taarifa. (alama 3)
"Tafadhali, nifungulie mlango sasa. Nitanyeshewa na mvua." Mtoto akamwambia.
Mtoto aliomba/alisihi afunguliwe mlango wakati huo kwa kuwa angenyeshewa na mvua.

(m) Andika katika ukubwa. (alama 2)
Mwanamwari huyu alijinunulia viatu vya ngozi.
Janajali hili lilijinunulia majiabu ya gozi/magozi.

(n) Andika matumizi mawili ya mshazari. (alama 2)
Kumaanisha au/ama
Kuandika visawe – baba/abu
Kuandika tarehe – 1/7/15

(o) Eleza matumizi ya neno mzee katika sentensi zifuatazo (alama 2)
(i) Baba mzee amelewa - kivumishi
(ii) Mzee amelewa - Nomino

(p) Tumia neno 'kuwa' kama kitenzi kishirikishi kikamilifu katika sentensi (alama 1)
Baba amekuwa mgonjwa. Hakiki sentensi.
Mama alikuwa mwalimu. Tanb. Neno hili lisitumiwe kama kitenzi kisaidizi.

(q) Tumia amba katika sentensi ifuatayo (alama 2)
Alaye ndiye aliaye
Ambaye hula ndiye ambaye hulia.

**ISIMU JAMII (Alama 10)**

(a) Eleza tofauti kati ya kuchanganya ndimi na kuhamisha ndimi. (alama 2)

ii). Kuchanganya ndimi – hali ya kutumia zaidi ya lugha moja katika mawasiliano . matumizi haya hujikita katika sentensi moja / mzungumzaji anatoka kidogo katika lugha moja na kuingilia nyingine kasha akarejelea lugha awali.

Kuhamisha ndimi – kubadilisha mkondo wa mazungumzo kutoka lugha moja hadi nyingine ambapo msemaji ana umilisi wa zaidi ya lugha mbili. (2 × 1 = 2)

(b) Andika sababu nne za kuchanganya na kuhamisha ndimi. (alama 4)

- Kupungukiwa na msamiati wa kutumia
- (ii) Kujitambulisha na kundi fulani la watu mf waliosoma, wanahirimu n.k
- Kujihusisha na lugha inayoenewa fahari
- Kutaka kuonyesha kuwa una uwezo wa kutumia lugha mbili au zaidi
- Kutaka kufafanua dhana fulani k.m uyoka (x-ray) Zozote 4 x 1 = 4

(c) Kiswahili ni lugha ya kibantu kulingana na ushahidi wa ki-isimu. Thibitisha kauli hii. (alama 4)

- Kufanana kwa msamiati km. ulimi (kisw) , Rurimi (kikuyu) lulimi (kibukusu)
- Maneno ya Kiswahili yana viambishi km yale ya kibantu mf. M-tu (Kiswahili) , Mu-ntu (zulu), mu-undu (kikuyu)
- Mpangilio wa maneno mf. Mtu mmoja (Kiswahili)
- Mundu umwe (Kikuyu), Muntu umwe (Kimeru)
- Muundo wa maneno kufanana – hutamkwa kisilabi
- Muundo wa maneno kuishia kwa irabu Zozote 4 x 1 = 4